D5

Ni nini iliyo katika hatari kuu?

- Wakati wa mkasa, jambo muhimu ni kuokoa maisha ya watu. Hata hivyo bidhaa au vitu fulani vyaweza kuwa muhimu. Mali hii yaweza kujumuisha vitu vya thamani, mifugo, mimea, ghala la vyakula, miti ya matunda, vyanzo vya maji, na vitu vingine vya kuimarisha uwezo wa kiuchumi, kama vile zana muhimu, vifaa vya uvuvi, vyombo vya usafiri na kawi.

- Watu wa kila aina wataweza kuwa na vifaa vya kila aina wanavyoona kuwa muhimu, ni muhimu sana kujadili na kutambua vitu muhimu wakati wa dharura. Ni muhimu pia kutambua na kujadili kuhusu vitu vinavyochukuliwa na jamii nzima kuwa muhimu wakati wa dharura.



Majadiliano D5

- Gawa wanachama katika makundi na kusoma hadithi hii kwa sauti:

Umeamka na kupata nyumba yako ikiteketea. Paa lote linateketea, hakuna jambo unaloweza kufanya ili kuokoa nyumba yako. Hakuna mtu mwingine ndani ya nyumba hiyo. Umesalia tu na dakika mbili au tatu za kuchomoka ndani ya nyumba hiyo huku ukiokoa vitu vitano muhimu. Ni vitu gani utakavyotoka navyo?

- Wacha muda fulani ili watu waweze kutafakari juu ya vitu vitano muhimu ambavyo wataokoa.

- Kisha hapo baadaye uliza kila kikundi kuhusu vitu vitano muhimu na mbona vitu hivyo.

- Toa wito kwa makundi tofauti kuorodhesha vitu walivyoona kuwa muhimu na sababu zilizowafanya kuchagua vitu hivyo.

- Eleza kwamba wamefanya uamuzi wa kutayarisha orodha. Kutoka kwa mali yao yote, wameweza *kutambua* vitu vitano vilivyo muhimu. Kisha baadaye wakaweza kutoa sababu za kuorodhesha.

- Baada ya kundi kujadili umuhimu wa orodha yao, uliza iwapo vitu hivyo vitakuwa na umuhimu kwa jamii? Je, watabadili orodha?

- Rudia zoezi hili ili kutambua vitu vya thamani katika jamii. Ufuatao ni mfano mwingine:

Umesikia katika matangazo ya radio kwamba kimbunga kinatarajiwa kutokea na kusababisha upepo mkali na mafuriko katika eneo lenu katika muda wa saa moja. Fikiria kuhusu jamii yenu na mambo matano muhimu mtakayotekeleza ili kuokoa watu wengi pamoja na mali yao. Ni jambo lipi litakalo pewa kipao mbele?

Jedwali hili latoa mifano ya mambo muhimu ya kuzingatia iwapo kimbunga kitatokea.

Kipao mbele
Huduma ya usafiri
Jumba au chumba cha dharura
Madawa
Maji masafi
Stakabadhi muhimu
Vitu vya dhamani kuu
Paa imara

D6

Jamii yaweza kuletwa pamoja kwa njia zipi?

- Kila eneo lina makundi ya kijamii na viongozi, maafisa rasmi na wasio rasmi. Utawala wa mikoa au serikali za mitaa na mashirika yaliyo sajiliwa yaweza kutoa uongozi na miongozo, lakini kwa wakati fulani jamii yaweza kukosa imani katika utawala.

- Makundi katika jamii yaweza kujumuisha makundi ya kujitegemea, makundi ya ushirika na uuzaji, makundi ya kidini, makundi ya vijana na jamii au tabaka. Baadhi ya makundi haya yaweza kuwa na ujuzi na maarifa ambayo yaweza kuwa muhimu sana wakati wa maafa.

- Baadhi ya watu waweza kuwa na talanta ya uongozi katika jamii, kwa mfano wakuu wa shule, wazee, wakunga au wahudumu wa afya. Watu kama hao wako na hekima na ujasiri. Watu wengi watawarejelea wakati wa matatizo ili kupewa ushauri. Hawa ndio watu wanaotoa mwelekeo wakati wa dharura.



Majadiliano D6

- Orodhesha viongozi walio katika jamii au eneo lako, viongozi wa serikali na wasio wa serikali. Wakati wa dharura, au taharuki na maelezo yanapo kanganya na kutolewa na viongozi kama hao, ni mkondo upi unaotakiwa kufuatwa?

- Ni ujuzi gani walio nao viongozi hawa katika kuwaleta watu pamoja? Ni tajriba zipi walizo nazo katika kuwaleta watu pamoja na kutoa mipango? Ujuzi huo waweza kuendelezwa kwa njia zipi ili kusaidia wakati wa dhiki?

- Viongozi hao wako na ushirikiano upi wa karibu na serikali? Ushirikiano kati ya wahudumu wa serikali, viongozi wa kidini na mashirika yasiyo ya serikali waweza kuimarishwa na kuendelezwa kwa njia zipi?

- Makundi ya kidini yaweza kuimarishwa na kuelimishwa kwa njia zipi ilikutayarisha wanachama kwa jukumu la uongozi? Hayo majukumu yaweza kuimarishwa kwa njia zipi?

D7

Ramani ya jamii

- Baada ya watu kutambua umuhimu wa kujiandaa ili kukabili janga, ni muhimu sana kutayarisha ramani ya eneo la jamii. Ramani hutoa fursa kwa yeyote kutazama na kutambua eneo lake. Ramani yaweza kuwasilisha ujumbe muhimu na kuonyesha jinsi vitu fulani vinavyolingana; kwa mfano, mijengo duni katika eneo linalokumbwa na mafuriko mara kwa mara, au kisima kilicho karibu na nyumba za watu matajiri. Ramani zilizo chorwa na makundi katika jamii kama vile vijana, wanaume au wanawake au hata wazee zaweza kuonyesha tofauti kubwa za kuvutia.

- Ramani zaweza kuchorwa kwenye ardhi, kwa kutumia vijiti, matawi na mawe kuwakilisha vitu fulani au kwa kutumia karatasi na kalamu. Ni muhimu kwa kundi kutambua vitu muhimu kama vile mto, vyanzo vya maji, miti, zahanati au vituo vya afya, shule, kanisa msikiti au barabara. Ni muhimu pia kutambua maeneo ya hatari kama vivuko dhaifu vya mto, daraja, visima vilivyo wazi na maeneo ya maporomoko ya ardhi.

- Toa changamoto kwa kila kundi kutoa maoni na mapendekezo. Baada ya kila kundi kuchora ramani yao, walete pamoja na kujadiliana kwa marefu na mapana.



Majadiliano D7

- Tenga siku moja ya kuandaa ramani ya eneo. Jukumu hili hutekelezwa vyema iwapo litahusisha kati ya watu 10 na 20. Watu wa kila umri wadogo kwa wakubwa, wanaume kwa wanawake wote watatekeleza jukumu muhimu. Waweza kuchanganya makundi hayo, au kukubali kila kundi kuchora ramani yao. Kwa mfano, watoto, wanawake, wanaume na wazee waweza kuchora ramani zao.

- Ni nini umuhimu wa kutayarisha ramani ya eneo la jamii?

- Ni kwa nini kila kundi, vijana, wanawake au wanaume kutoa mapendekezo tofauti tofauti kwenye ramani? Ni mbinu zipi zitakazotumiwa kujumuisha maoni hayo yote kwa pamoja? Ni maoni yapi au ya akina nani yaliyo muhimu zaidi?

- Mapendekezo hayo yaweza kushirikishwa na kujumuisha kwa mbinu zipi ili kutumiwa?

- Je, kuna aina fulani ya kitu ambacho kilitambuliwa na kila kundi? Ni kitu gani hicho? Mbona kundi fulani laweza kutambua vitu fulani?

Miundo msingi

Wakati wa dharura hakuna nafasi au muda wa kuandaa miundo msingi. Jamii yapaswa kutumia rasilmali zilizoko kwa wakati huo. Eneo la kutoa maji masafi kwa matumizi, huduma za afya, chakula, mahali pa kujikinga ni baadhi ya miundo msingi na rasilmali za kupewa umuhimu wa kwanza.

Baada ya kukadiri hayo yote, tafakari kuhusu rasilmali zilizoko:

- Vyanzo vya maji ambavyo havitumiwi kwa wingi katika maeneo ya mwinuko au maeneo yaliyobadilishwa na kutiwa bomba au tanki. Labda kuna majengo ya kudumu yaliyo mbali na kijiji au mji ambayo yaweza kukarabatiwa na kutumiwa kama vituo vya dharura wakati wa jangwa.

- Upanzi wa miti ni jambo la faida nyingi. Miti ni chanzo cha kuni na vifaa vya ujenzi. Miti husaidia katika kuimarisha umbo la mchanga na kuzuia mmomonyoko wakati wa mafuriko. Miti husitiri eneo dhidi ya kimbunga au hata mafuriko. Iwapo miti itapandwa kando ya barabara, basi itakuwa ni alama ya mahali palipo na njia wakati wa mafuriko.



Majadiliano D8

- Tafakari kuhusu hatima ya baada ya mkasa wa aina yeyote: mafuriko, kimbunga, moto, mazao duni, janga la kuzuka kwa magonjwa ya mifugo, mtetemeko wa ardhi au hata vita. Kwa kila tukio tafakari kuhusu muda na jinsi watu walivyokabili na mahitaji muhimu.

- Katika maeneo ya umaskini hatuwezi kuwa na rasilmali za kutosha, hata hivyo kila jamii ina rasilmali. Tafakari kuhusu aina ya rasilmali zilizo katika jamii yenu.

- Tafakari kuhusu mahali ambapo jamii yaweza kupata maji ya kutosha iwapo sehemu za kawaida zimeharibiwa. Kuwepo kwa maji masafi ni jambo la dharura linalopaswa kupewa umuhimu wa kwanza.

Kuimarisha ujuzi wa watu

- Wakati wa dharura ujuzi wa kila aina huhitajika, hata hivyo hamaki au taharuki yaweza kusababisha matatizo mengi au michafuko. Ni muhimu sana iwapo kuna kundi la watu wenye ujuzi wa kila aina utakao faa wakati wa dharura. Watu waliokomaa waweza kuwa na hekima. Watu waweza pia kupata mafunzo ambayo watahitaji kujihami na kutumia.
- Ujuzi na maarifa yaweza kujumuisha kuandika rekodi, kuleta watu pamoja, kuandaa na kuelekeza watu ili kutekeleza kazi au jukumu fulani kama vile ujenzi wa choo, vyumba, mifereji ya maji, kuendesha gari, shughuli za maakuli na utunzaji wa hazina. Katika maeneo ya mafuriko, watu walio na ujuzi wa kuogelea na kutunza mitumbwi. Watu wazee waweza kuwa na utaalamu wa kutayarisha madawa ya kiasili, au vyakula vya kiasili.

Majadiliano D9

- Ni ujuzi wa aina gani unaohitajika katika jamii? Ni vikwazo vipi vinavyokumba juhudi za kuelimisha na kufahamishana?
- Ni mbinu gani zinazoweza kutumiwa ili kushirikiana na kufahamishana katika kujifunza ujuzi fulani?
- Ni maarifa yapi yanayoweza kujengwa? Kwa mfano, watu katika eneo hilo wananaweza kuogelea, hali kadhalika kuna ujuzi wowote wa kuokoa wahanga wa mafuriko? Ni nani anayeweza kutoa mafunzo kuhusu mbinu za uokozi?
- Ni majukumu yapi yanayoweza kutekelezwa ili kufahamisha na kufundisha jamii hasa utaalamu wasio nao? Kwa mfano, je, vikao vya mafunzo ya Huduma ya Kwanza vyaweza kuandaliwa? Je, vijana waweza kuhimizwa kuchukua taaluma ya urekebishaji wa magari au ujenzi kwa jumla?

Mbiu ya mgambo

Wakati wa mkasa au janga linapozuka, watu hutaka kupokea habari muhimu, uvumi na taarifa zisizofa huweza kuzua taharuki na hofu kwa wakaazi. Habari za kuaminika hufa sana. Vituo vya radio, wahudumu wa serikali au mashirika yasiyo ya serikali yaweza kutegemewa kwa kutoa habari na misaada baada ya mkasa. Ni bora kuandaa mbinu ya kuwasilisha ujumbe kwa makini na haraka iwezekanavyo.

- Kila aina ya jamii hutumia vifaa vya kila aina katika kuwasilisha ujumbe. Vyombo vya kupasha habari vyaweza kuwa ngoma, ili kueleza ujumbe kuhusu kifo, kengele kama zile za shule au za kanisa, aina nyingine za kutoa mbiu.

- Je, kuna vifaa vyovyote vya kupaaza sauti vinavyotumiwa kuwasilisha ujumbe wakati wa dharura ili kuwaita watu pamoja? Jadili kuhusu mbinu bora za kuita umati mkubwa au kutoa tahadhari na ujumbe wa kuokoa maisha.

Majadiliano D10

- Je, kuna vifaa gani katika eneo lenu vinavyoweza kupaaza sauti za kutoa ilani au tahadhari? Je kuna vifaa vingine vya mgambo kama vile, pembe? Kuna kanisa au msikiti ulio na vyombo kama vile kengele?

- Jenga uhusiano mwema na vituo au kituo cha radio kilicho karibu na eneo lako. Ni akina nani wanaopaswa kuchukua jukumu la kuwasiliana na kituo hicho kwa matangazo? Ni ujumbe wa aina gani unaopaswa kutangazwa kupitia kwa kituo hicho? Habari za kutegemewa zaweza kupatikana wapi?

- Katika maeneo mengi ujumbe waweza kuwasilishwa kwa mdomo. Jadili jinsi mfumo huu waweza kutumiwa katika eneo lenu, na vyombo au zana mnazo weza kutumia kutoa ilani wakati wa dharura.

- Katika sehemu nyingi dini au madhehebu husaidia sana katika kuwasilisha ujumbe. Ni mbinu gani zinazotumiwa? Tunaweza kujifunza nini kutokana na haya? Mbinu hizo zaweza kutumiwa vipi katika kuwasilisha ilani au jambo la dharura?

- Jamii fulani kule Filipino hufunga kamba kupita juu ya mito na kufunga bendera na kengele kwenye kamba hiyo. Iwapo kiasi cha maji kwenye mto huongezeka, maji hupitia kwenye bendera na kasi yake kufanya kengele kulia. Waweza kufikiri kuhusu mbinu nyingine za kutoa ilani?

- Ni bora kuandaa kituo cha kujiandikisha ili kufahamu na kutambua watu ambao hawajulikani walipo na pia kutoa ripoti kuhusu hatima yao. Shule na mijengo ya dini ni vituo vinavyoweza kutumiwa na kupata watu watakao andikisha na kutekeleza utaratibu wa kufahamisha. Je, ni vipi mtakavyo fahamisha watu kuhusu kituo hicho?

Mijengo ya jamii

Katika kila eneo kuna mijengo ya jamii inayotoa huduma muhimu kwa wakaazi kama vile shughuli za kidini. Majengo kama haya yapaswa kuwa salama, kwa sababu ya umati mkubwa unaotegemea, na pia kama kimbilio wakati wa janga.

- Zingatia jengo lolote kubwa karibu na jamii, kama vile shule, kanisa, msikiti, majumba ya mikutano au ofisi ambayo yaweza kuwekwa katika kundi hili. Majengo yanayo nuiwa kutumiwa ili kunusuru wahanga wa mafuriko yapaswa kujengwa katika sehemu za mwinuko. Jengo kama hilo huhitaji paa lililo na uwezo wa kukabili kimbunga.

- Mikutano ya jamii yaweza kujadili kuhusu mbinu za kuboresha mijengo kama hiyo. Kwa mfano, idadi fulani ya madarasa katika shule kuchaguliwa. Makundi ya jamii yaweza kushirikiana ili kuboresha madarasa hayo. Tanki kubwa la maji laweza kujengwa. Vyoo vya shule vyaweza kujengwa na kuboresha. Kabati dhabiti yaweza kuongezwa ili kuhifadhi zana za dharura.

Majadiliano D11

- Usalama wa majengo ya uma waweza kuimarishwa kwa njia zipi? Mijengo kama hiyo yaweza kuhimili mafuriko, moto, au kimbunga? Mtaalamu au mhandisi aweza kukagua mijengo?

- Jadili kuhusu vifaa au zana muhimu mnazoweza kuzingatia katika chumba cha kushughulikia mkasa, huku mkizingatia maafa ambayo yaweza kukumba eneo lenu.

- Ni vifaa vya aina gani vinavyoweza kuhifadhiwa katika chumba cha dharura? Zana hizo zaweza kujumuisha vitu kama tochi, mshumaa, mafuta, vibuyu, mitungi, viberiti, plastiki, vyakula na maji, radio ndogo na betri. Kati ya vifaa vilivyotajwa, ni vigani vilivyo muhimu na ni vipi vinavyoweza kukusanywa nyakati za mwisho kabla ya kukumbwa na janga (ukitilia maanani kwamba onyo la tahadhari limetolewa kabla ya mafuriko au kimbunga)?

- Ni nani atakaye pewa jukumu la kuweka kifunguo cha kabati au chumba cha dharura? Ni nani atakaye pewa mamlaka ya kukagua tanki la maji lililojengwa kwa ajili ya jamii?

- Jamii yaweza kufanya ukaguzi wa jumba la uma kukadiri usalama au hatari yeyote? Tazama vitu kama mahali pa kupitia au kuingilia, nyaya za umeme zilizo wazi mlango uliovunjika au hali ya kuta. Zingatia mambo ya dharura kama vile kuinua na kuweka nyaya za umeme juu katika maeneo yanayokumbwa na tisho la mafuriko.

- Tutakuwa na nafasi ya kutosha? Mahitaji maalum ya akina mama na watoto yaweza kushughulikiwa?